

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**MKOA WA DODOMA**  
Tel.: +225 262321569  
Fax: +225 262322650



Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,  
P.O BOX.1249,  
**DODOMA.**  
E-mail: md@dodomamc.go.tz

Tarehe: 29/05/2018

**TANGAZO LA ZABUNI**

**ZABUNI Na. LGA/020/2018--2019/NCS/1-8**

**ZABUNI ZA WAKALA WA UKUSANYAJI WA MAPATO KATIKA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

1. Halmashauri ya Jiji la Dodoma inakusudia kuweka mawakala wa kukusanya Mapato kwa kupangisha maeneo mbalimbali ya kufanyia biashara kwa kipindi cha kuanzia **Julai, 2018** hadi **June, 2019**.
2. Halmashauri ya Jiji ya Dodoma inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, mashirika, taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuingia mikataba ya kukusanya mapato/kupangisha kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

<b>Na.</b>	<b>CHANZO CHA MAPATO</b>	<b>NAMBA YA ZABUNI</b>
1	Upangishaji wa banda la kuku lililoko Miyuji	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/1</b>
2.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa ulioko soko la Majengo	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/2</b>
3.	Upangishaji wa ghala la DODIDECO	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/3</b>
4.	Uendeshaji wa huduma ya choo ya kulipia kilichopo soko la Majengo	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/4</b>
5.	Ukusanyaji wa ada ya Maegesho ya magari (magari binafsi, malori, pickups na taxi) isipokuwa ndani ya eneo la stendi ya mabasi)	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/5</b>
6.	Upangishaji na uendeshaji wa mgahawa ulioko eneo la Nyerere Square	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/6</b>
7.	Ukodishaji wa vibanda 30 (thelathini) vya soko la Majengo vilivyoko wazi (havina wapangaji)	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/7</b>
8.	Upangishaji wa eneo la wazi karibu na Chuo cha Biashara (CBE)	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/8</b>

3. Zabuni hii itaendeshwa katika taratibu za mfumo wa Ushindani wa Kitaifa (National Competitive Bidding) kama ilivyoelekezwa katika Kanunni za Ununuzi zilizotolewa kwa tangazo la serikali namba 446 la mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 isipokuwa itakapokuwa imeandikwa vinginevyo kwenye masharti maalum ya uombaji (Bid Data Sheet).
4. Weneye nia ya kuomba zabuni hii wanaweza kupata taarifa za ziada na kukagua nyaraka za zabuni katika ofisi ya Katibu – Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Jiji la Dodoma Mkao Makuu, ghorofa ya kwanza, chumba namba 14, S. L. P. 1249, Dodoma, kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 mchana, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko ya ki-Taifa.
5. Weneye nia ya kuomba zabuni hii wanatapata **Nyaraka za Zabuni** katika lugha ya Kiswahili baada ya kulipa ada ya **Shs. 100,000/= (shilingi laki moja tu)** ambayo haitarejeshwa (**non - refundable**). Malipo hayo yalipwe kwa **Mkurugenzi wa Jiji, Jiji la Dodoma, S. L. P. 1249, Dodoma.**
6. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe **11/06/2018** saa nne (4) asubuhi, na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kupokea zabuni hizo mbele ya waombaji watakao amua kuhudhuria kwenye ukumbi ya mikutano ulioko jengo la Makao Makuu ya Manispaa (zamani likijulikana kama jengo la CDA), ghorofa ya pili.
7. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ioneshwe namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-  
**Mkurugenzi wa Jiji,  
Jiji la Dodoma,  
S.L.P 1249,  
DODOMA.**
8. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa barua barua pepe (e-mail) hazitapokelewa.



Godwin E. Kunambi,  
**Mkurugenzi wa Jiji  
JILI LA DODOMA.**